JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE

03 **HISABATI**

Muda: Saa 1: 30 **Mwaka: 2022.**

Maelekezo



1. Mtihani huu una jumla ya maswali **matano (5)**
2. Jibu maswali **yote**

Katika swali la 1 – 5, kokotoa swali ulilopewa na kisha andika jibu sahihi kwenye nafasi iliyotolewa.

Na.		Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
1.	a)	Ana alipewa chungwa, akala $\frac{1}{4}$ ya chungwa hilo. Ni sehemu gani iliyobaki?		
	b)	Andika 99,001 kwa kirefu		
	c)	Thamani ya namba X katika namba XVIII ni		

Na.		Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
	d)	Andika kwa kirumi namba iliyopo kati ya 48 na 50		
	e)	Ni namba gani itajumlishwa na 4,392 ili kupata 7,005?		
2.	a)	Hatua moja ya kobe ni sm 5. Je, atatembea hatua ngapi kufikia sm 30?		
	b)	Juliasi ana watoto watano wanaopishana umri kwa miaka 5 kila mmoja. Ikiwa mtoto wa kwanza ana miaka 35, je mtoto wa nne ana umri gani?		
	c)	Nchi nne zilipata uhuru wao kama ifuatavyo: Kenya 1962, Tanganyika 1961, Uganda 1963 na Zimbabwe 1980. Je, ni nchi ipi ilikuwa ya kwanza kupata uhuru?		
	d)	Matokeo ya Gladness ya majaribio ya mwezi yaliongezeka kwa alama 12 kila mwezi. Ikiwa mwezi wa kwanza alipata alama 186, je, mwezi wa nne alipata alama ngapi?		

Na.		Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
	e)	Shule ya msingi Mji mpya huchagua viongozi wake kila baada ya miaka 2. Ikiwa uchaguzi wa mwisho ulifanyika mwaka 2018, uchaguzi unaofuata ulifanyika mwaka gani?		
3.	a)	Tafuta tofauti ya 39,365 na 33,868		
	b)	Aisha amegawanya maembe 350 katika mafungu 10 yenye idadi sawa. Je, kila fungu lina maembe mangapi?		
	c)	Baraka hulipwa shilingi 4,000 kwa siku. Ikiwa anafanya kazi kwa siku 40, jumla atalipwa shilingi ngapi?		
	d)	Joel alinunua redio na kuiuza kwa shiingi 60,500. Ikiwa alipata faida ya shilingi 20,000, je, aliinunua redio hiyo kwa shilingi ngapi.		
	e)	Kuku huatamia mayai kwa muda wa siku 21. Je, muda huo ni sawa na majuma mangapi?		

Na.		Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
4.	a)	Panga vipimo vifuatavyo kuanzia kikubwa hadi kidogo: m 900, sm 2, km 3 na mm 400		
	b)	Kipi ni kirefu zaidi kati ya waya wa sentimeta 20 na uzi wa meta 2?		
	c)	Kuna vipande vingapi vya mstari katika mstari ufuatao?  		
	d)	Tafua mzingo wa pembetatu ifuatayo:  		
	e)	Mzingo wa mraba n ism 196. Tafuta urefu wa upande mmoja		
5.		Jedwali lifuatalo linaonesha idadi ya wanafunzi waliomaliza darasa la saba katika shule ya msingi Muungano kwa miaka mine: **Mwaka** | **Idadi ya Wanfunzi** 2014 | 80 2015 | 90 2016 | 95 2017 | 98		

Na.		Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
	a)	Mwaka gani wanafunzi wengi zaidi walimaliza darasa la saba?		
	b)	Jumla ya wanafunzi wangapi waliza daras la saba mwaka 2014 na 2015?		
	c)	Mwaka upi wanafunzi wachahce zaidi walimaliza darasa la saba?		
	d)	Tafuta tofauti ya idadi ya wanafunzi waliomaliza mwaka 2014 na 2017.		
	e)	Je, jumla ya wanafunzi wangapi walimaliza shule katika hiyo miaka minne?		